# STD 7 END TERM 3 EXAM 2019

## KISWAHILI

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.***

Upepo __1__ ulivuma na kunituliza __2__ ulikuwa __3__ nilale pale chini ya mti. Hiyo ilikuwa baada ya kutwa __4__ ya kufanya kazi za __5__ ambazo hazikuweza __6__ mahitaji yangu kikamilifu. Mara kilio __7__ kikapasua anga na kuuharibu utulivu uliokuwapo. Nilisimama wima kuifuata sauti ile nikifahamu kuwa __8__.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. nzuri | B. mwanana | C. mpole | D. mzito |
| 2. | A. kama kwamba | B. ni kama | C. maadamu | D. hususan |
| 3. | A. umetaka | B. unataka | C. ukitaka | D. ulitaka |
| 4. | A. mzima | B. kucha | C. kuchwa | D. nzima |
| 5. | A. ujira | B. shokoa | C. kijungujiko | D. sulubu |
| 6. | A. kuitosheleza | B. kuzitosheleza | C. kutosheleza | D. kuyatosheleza |
| 7. | A. ukali | B. vikali | C. kali | D. kikali |

8. A. mbiu ya mgambo ikilia kuna jambo
   B. chelewa chelewa utapata mwana si wako
   C. ukistaajabu ya Musa utayaona ya Firauni
   D. mti hauendi ila kwa nyenzo

Neno 'mihadarati' __8__ tu msamiati niliousikia shuleni __10__ siku moja nilipokumbana nayo __11__. Nilipatana na unga __12__ kwenye chumba cha ndugu yangu nikitafuta mpira wangu. Bila kujua, nilichukua __13__ moja na kuonja. Hisia zilizofuata ziliwiana kabisa na maelezo ya mwalimu wetu wa somo la __14__ . __15__ baba ili nipate huduma ifaayo.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 9. | A. ilikuwa | B. ulikuwa | C. lilikuwa | D. yalikuwa |
| 10. | A. kutoka | B. hata | C. tangu | D. hadi |
| 11. | A. bega kwa bega | B. ana kwa ana | C. ima fa ima | D. unyo kwa unyo |
| 12. | A. mweupe | B. nyeupe | C. weupe | D. eupe |
| 13. | A. finyo | B. tumbi | C. biwi | D. funda |
| 14. | A. Dini | B. Sayansi | C. Kiingereza | D. Hisabati |
| 15. | A. Nilikimbiwa | B. Nilikimbilia | C. Nilimkimbilia | D. Nilimkimbia |

***Kutoka swali la 16 hadi 30, chagua jibu sahihi kulingana na maagizo uliyopewa.***

16. Chagua sentensi iliyo sahihi kisarufi.
    A. Madarasani humo mlimofagiliwa ni kuzuri.
    B. Madarasani hayo yaliyofagiliwa ni mazuri.
    C. Madarasani huko kulimofagiliwa ni kuzuri.
    D. Madarasani humo mlimofangiliwa ni mzuri.

17. Teua sentensi yenye kivumishi halisi.
    A. Runinga nyeusi zimeuzwa kwa wingi.
    B. Mpigambizi hodari aliopoa miili iliyozama.
    C. Timu yetu imepokea tuzo nyingi.
    D. Wasikilizaji hawajaipenda sauti yenyewe.

18. Ni neno lipi lililonyambuliwa vyema katika kauli ya kutendesha?
    A. Nawa - Naza
    B. Iga - Igisha
    C. Lala - Lisha
    D. Lia - Liza

19. Ni kundi lipi lenye vyombo vya uchukuzi?
   A. Rukwama, matwana, pantoni.
   B. Manowari, sime, mishale.
   C. Nyundo, randa, bisibisi.
   D. Iliki, halua, mdalasini.

20. Mtoto wa sungura huitwa
   A. shibli  B. maige
   C. kisuse  D. kitungule.

21. **Eleza maana ya sentensi hizi**:
   Mwanafunzi hakufanya mtihani.
   Mwanafunzi hakufuzu.
   A. Mwanafunzi angefanya mtihani angefuzu.
   B. Mwanafunzi hangefanya mtihani hangefuzu.
   C. Mwanafunzi asingefanya mtihani asingefuzu.
   D. Mwanafunzi hakufanya mtihani kwa sababu hakufuzu.

22. Mbona punda hutandikwa **kwa** mijeledi?
   Kwa imetumika kuonyesha
   A. sababu  B. ala
   C. kitendo  D. kihusishi

23. Umoja wa "Mifenesi imekatwa yote' ni
   A. Mafenesi yamekatwa yote.
   B. Fenesi limekatwa lote.
   C. Mfenesi umekatwa wote.
   D. Mfenesi imekatwa yote.

24. Chagua methali iliyo tofauti na nyingine.
   A. Haraka haraka haina baraka.
   B. Polepole za kobe humfikisha mbali.
   C. Aliye juu mngoje chini.
   D. Polepole ndio mwendo.

25. '**Maadamu**' ni sawa na
   A. pengine  B. kwa sababu
   C. mara nyingine  D. bila ya

26. Teua sentensi iliyotumia **ji** kuonyesha hali.
   A. Usomaji wa Rashid unasisimua.
   B. Jifya moja haliinjiki chungu.
   C. Mtoto alijikata kwa wembe.
   D. Mchezaji aliyeumia yu hatarini.

27. Chaurembo ana **nywele nyingi ndefu** kichwani pake. Maneno yaliyopigwa mstari ni sawa na
   A. kishazi  B. kikonyo
   C. shada  D. kivunga.

28. Sitiari imetumika katika sentensi ipi miongoni mwa hizi?
   A. Fidhuli amevimba kichwa siku hizi.
   B. Maji haya ni barafu, hayanyweki.
   C. Pombo na pambo hawapikiki katika chungu kimoja.
   D. Mwalimu wetu anapendeza kama malaika.

29. Wanawake walioolewa na mume mmoja huitana
   A. wifi  B. shemeji
   C. mwanyumba  D. mkemwenza

30. **Baadilisha sentensi hii katika udogo**:
   Jina lake ni refu.
   A. Kijijina chake ni kirefu.
   B. Majina yao ni marefu.
   C. Kijijina chake ni ndefu.
   D. Kijina chake ni kirefu.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Pilikapilika zinazokuwapo kabla ya mabarobaro kwenda jandoni huwa za nyuki mzingani. Ninakumbuka vyema niliyopitia kabla ya kukipitia kisu kikali cha ngariba. Maandalizi yenyewe yalifaa kung'oa nanga kabla ya muda usiopungua fungate moja. Nilielezwa kuwa kusudi huwa kupata baraka kutoka kwa watu mbalimbali na nasaba yako. Aidha, humwezesha mhusika kujiandaa kiakili na kimwili kabla ya siku ya siku.

Nilifungiwa njuga mguuni na kukabidhiwa chuma fulani kidogo ambacho ningekigongagonga katika safari zote. Nilifaa kuwatembelea wajomba, shangazi, ami, hale na wavyele wa wazazi wangu. **Safari yenyewe ilikuwa ya nyayo kuchuana na lami.** Mwimbaji hodari mwenye tajriba na uzoefu wa mambo haya alitafutwa na shughuli nzima ikaanza. Tulitoka nyumbani macheo hiyo tukiwa watu wanne pekee lakini baada ya hatua kadhaa, wanakijiji walikuwa wameitikia wito wa mbiu na kujiunga nasi. Ilikuwa **mwiko** kwa yeyote wa jinsia ya kike kujiunga na kundi hilo ikidhaniwa kuwa angeleta baa kwa yule ambaye angechunwa jogoo.

Hatimaye, siku iliyokuwa imesubiriwa kwa hamu na hamasa [illegible] hodi. Ilikuwa siku ya ndovu kumla mwanawe kwa sababu kitongoji kizima kingesimamisha shughuli zote kushuhudia vijana wake wakidhihirisha ukomavu wao. Wale waliotoa machozi kwa kutostahimili uchungu wangeitwa waoga milele. Macho makavu wakati wa tohara ilikuwa ish[illegible] ya ujasiri na udume.

Tuliamshwa [illegible] na nyimbo za siku hiyo maalum zikaanza [illegible]. Kila [illegible] isipokuwa sisi wa **kushu**[illegible] [illegible] na [illegible] isiyo na kifa[illegible] [illegible] kwa mbali nili[illegible] [illegible] yetu [illegible] isipokuwa Dumberi am[illegible] [illegible] ha hi[illegible] kwa h[illegible] [illegible] tukavaa

suti ya Mungu na kusukumwa majini. Mwili ulizizima moja kwa moja. Baada ya dakika kadhaa nilizoona kama mwaka mzima, tulipakwa matope mwilini pote na tukapelekwa kutimiza malengo ya mila za jamii yetu.

Kisu kilipopenya kwenye ngozi zetu hatukutokwa na tone hata moja la machozi. Pia, damu haikuvuja mno kutokana na shughuli zilizotangulia siku hiyo.

**31.** Mwandishi anaanza kisa hiki kwa maelezo kwamba
- A. shughuli zote za jandoni ni za nyuki mzingani
- B. pilikapilika za vijana kuingia jandoni huwa nyingi
- C. shughuli huwa nyingi wavulana wakingoja kuingia jandoni
- D. mabarobaro huingia na kutoka jandoni kama nyuki.

**32.** Ngariba hufanya kazi ya
- A. kunoa visu vyenye makali
- B. kuwapasha wavulana tohara
- C. kufua visu
- D. kuwafundisha vijana jandoni.

**33.** Sababu za kuanza maandalizi mapema ni
- A. kupata ujasiri na pia kubarikiwa na nasaba
- B. kupata baraka za Mungu na kujiandaa kiakili na kimwili
- C. kupewa zawadi na kubarikiwa na watu wa ukoo
- D. kupashwa tohara na kukomaa.

**34.** Kifungu **'safari yenyewe ilikuwa ya nyayo kuchuana na lami'** kinamaanisha
- A. ilikuwa safari ya kuchosha
- B. wangeepuka njia ndefu za lami
- C. safari ilikuwa ndefu.
- D. wangesafiri kwa miguu.

**35.** Kilichowavutia wanakijiji kujiunga na kundi la mwandishi ni
- A. kelele zilizokuwa mtoni
- B. miondoko mizuri ya kucheza
- C. nyimbo zilizokuwa zikiimbwa
- D. sauti iliyotoka kwenye mbiu.

**36.** Methali inayoweza kutumiwa badala ya maneno ya mwanzo wa aya ya tatu ni
- A. mgeni njoo mwenyeji apone
- B. siku njema huonekana asubuhi
- C. hayawi hayawi huwa
- D. kuenda mbele si kurudi nyuma.

**37.** Ujasiri wa msimulizi na wenzake ungedhihirika iwapo
- A. wasingestahimili uchungu
- B. mmoja wao angelia
- C. wangeshindwa kuzuia machozi
- D. wangeyazuia machozi.

**38.** Hisia za msimulizi katika aya ya nne zilitokana na
- A. woga aliokuwa nao
- B. mawazo ya kupashwa tohara
- C. yaliyokuwa mbele yao
- D. kudundwa na moyo.

**39.** Neno **'mwiko'** lina maana gani kulingana na kifungu hiki?
- A. Jambo la kawaida.
- B. Ubaguzi wa kijinsia.
- C. Kifaa cha kusongea ugali.
- D. Jambo lililopigwa marufuku na jamii.

**40.** Uvujaji wa damu ulidhibitiwa na
- A. kuwatosa watahiriwa majini alfajiri
- B. kisu kikali cha ngariba
- C. shughuli za siku iliyotangulia
- D. nyimbo za wanakijiji.

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50.</u>***

Binadamu hupitia hatua mbalimbali zilizo tofauti kabla ya kuifikia ya mwisho iliyo ya mauti. Azaliwapo **<u>huengwaengwa kama yai</u>** asije akaanguka na kujivunjilia mbali vifupa visivyo imara. Atalishwa baada ya kujinyonyea, aogeshwe, abembelezwe na kumulikiwa taa hadi atakapotimiza umri wa kuweza kujifanyia mambo. Baadaye hujipata akiwa katika umri wa kujitegemea na hapo ndipo anatengana na wazaziwe ili naye aanzishe familia na kuikimu.

Ukongwe uingiapo huja na changamoto zake ambazo huhitaji auni ya jamaa au hata jamii. [illegible]ndo wa kuwatelekeza wazee unaendelea kuwa wa kawaida katika jamii nyingi. Katika zama za [illegible]a, hawa ndio watu waliostahiwa kuliko yeyote. Hii ilichangiwa pakubwa na uwezo wao wa [illegible] suluhu na migogoro katika jamii. Wingi wa mvi [illegible] uliashiria utajiri mkubwa wa

hekima. Mvi ambazo zilitokana na safari ndefu katika bahari hii ya maisha. Nako kuishi kwingi kukawafanya kuona mengi. Ndipo wakasema wenyewe kuwa jungu kuu halikosi ukoko.

Labda mjo wa mahakama umechangia kuwasahau wazee wetu. Lakini ni mara ngapi wahalifu wameachiliwa huru kwa ukosefu wa ushahidi. Hujasikia visa vya watu kupatikana na hatia na kufungwa hata maisha licha ya kutovunja sheria zozote? Uzee ulithaminiwa kwa nasaha ambazo ziliwanyosha wanajamii. Ulipendwa kwa ngano tamu tamu zilizotolewa kwa wajukuu na vitukuu. Kupitia kwa ngano hizo tamaduni za jamii ziliwezwa kurithishwa kizazi hadi kizazi.

Sasa tunawabeza na kuwatupilia mbali. Kwa kweli asiyekujua hakuthamini. Serikali kwa kutambua kuwa kizazi hiki huenda kikaangamia, ilianzisha mpango wa kuwapa wazee fedha za kukidhia mahitaji yao. Aliyeuratibu mpango wenyewe anafaa kupongezwa kwa kuwa hakurejesha thamani yao tu bali aliiokoa jamii nzima inayoyumbayumba kwa kukosa misingi ya maadili. Watunzeni wazee kwani hamjui uzeeni mwenu mtatunzwaje.

41. Kulingana na kifungu hiki, kifo ni
   - A. mwisho wa hatua muhimu ipendwayo na binadamu
   - B. hatua mojawapo isiyopendwa na binadamu
   - C. hatua inayotamatisha maisha ya binadamu
   - D. hatua ya pekee katika maisha ya binadamu.

42. Ni katika hatua zipi ambapo mja huhitaji msaada wa wanajamii?
   - A. Utotoni na uzeeni
   - B. Ujana na ukongwe
   - C. Ujana na makamo
   - D. Utotoni pekee

43. Binadamu anatarajiwa kuanza maisha yake mwenyewe pale ambapo
   - A. anakuwa mkubwa kiumri
   - B. anaweza kujikidhia mahitaji yake
   - C. anatengana na wavyele wake
   - D. anaanzisha familia yake.

44. Ni jambo gani ambalo limekuwa mazoea kulingana na ufahamu?
   - A. Kuupuuza ujana.
   - B. Kuwatekelezea wazee majukumu.
   - C. Kuwadhamini wazee
   - D. Kuwapuuza vikongwe.

45. Taadhima kuu kwa wazee ilitokana na
   - A. kuwapo kwa mvi vichwani
   - B. serikali kuwapa mikopo
   - C. uwezo wa kuitatua migogoro
   - D. kuachwa bila uangalizi.

46. Kwa kusema '**Jungu kuu halikosi ukoko**' mwandishi anamaanisha
   - A. chombo kilichopikiwa lazima kiwe na mabaki ya chakula
   - B. wazee wana maarifa ya kutosha kukabiliana na changamoto za dunia
   - C. wanaofahamu kazi ya kufinyanga vyungu ni wazee
   - D. dunia haikosi matatizo kamwe.

47. Maneno '**huengwaengwa kama yai**' ni mfano wa
   - A. tashbihi
   - B. tashihisi
   - C. sitiara
   - D. semi.

48. Maswali yanayoulizwa katika aya ya tatu ni dhihirisho kuwa
   - A. korti nazo zina upungufu wake
   - B. mahakama zina ubaguzi
   - C. korti zimedhibiti uhalifu vilivyo
   - D. baadhi ya watu wamefungiwa kortini bila hatia yoyote.

49. Kwa mujibu wa aya ya mwisho
   - A. serikali inajua kuwa kizazi cha wazee kitaangamia
   - B. wazee wanafaa kuangamizwa kwani hawafai lolote
   - C. wazee wamepewa ajira na serikali
   - D. serikali imevalia njuga suala hili la uzee.

50. Mwandishi anatoa nasaha kuwa
   - A. mwenzako akinyolewa chako tia maji
   - B. ujana ni moshi ukienda haurudi
   - C. mbio za sakafuni huishia ukingoni
   - D. fimbo za mbali haiui nyoka.